www.ippmedia.com

# Alasiri Online

ISSN 0856 Na. 001 Jumamosi Aprili 6, 2019 Tanzani 500/- Kenya 50/-



# RIYANA AWAPA MAKAVU

## DUDU BAYA AJIRUDI

## NEDY AAMUA KUBEBA CHIPUKIZI

# CHID BENZ AKUBALI YAISHE

Na Mary Kadoke

INAONESHA Kwaresma imekuja na neema kwa wasanii kutoka Bongo Fleva, mfokaji Chid Benz naye ameamua kuwaomba radhi wote aliowahi kuwakosea hapo awali.

Akifanya mazungumzo na Alasiri Online mkali huyu wa ngoma ya Muda amesema haoni maana ya kuwekeana vinyongo kwani duniani wote ni wa kupita tu.

"Kama kuna mtu yeyote anahisi nimemkwaza na kumkosea, sidhani kama kuna ulazima wa kuwekeana vinyongo," amesema.

"Kikubwa ni kusameheana na kuacha maisha yaendelee maisha ni mafupi na bifu hazina maana," ameongeza.

Dudu Baya au Konki kama anavyojiita hivi karibuni aliamua kumuomba msamaha marehemu Rugemarila Mutahaba baada ya kutoa madai yake kuwa aliwahi kudhulumu.

Alichodai ni kwamba marehemu Ruge aliyekuwa mkurugenzi wa vipindi na uzalishaji wa Clouds Media Group pamoja na watangazaji wa kipindi cha Extra Extra Large (XXL) ni watu waliodai rushwa ili kurusha habari zake na wasanii wengine kwa ujumla.

Hata hivyo baada kufanya mazungumzo na Alasiri Online, alikiri kukosea na kumuomba msamaha marehemu Ruge pamoja na ndugu jamaa na marafiki juu ya kauli zake akidai kuwa kipindi hiki cha Kwaresma au mfungo si lazima kutunza vinyongo.





# RIYANA AWAPA MAKAVU

Na Anaeli Mbise

MUIGIZAJI wa filamu nchini Riyama Ally anakerwa na mtindo wa baadhi ya wasanii wa kutafuta umaarufu kwa kufanyiana vurugu.

Akizungumza na Alasiri Online, Riyama amesema msanii ni kioo cha jamii na anatakiwa kutambulika au kupata umaarufu kupitia kazi zake za sanaa anazozifanya na siyo zaidi ya hapo.

"Ninasema hivyo kwa sababu wapo baadhi yao siwataji majina, wanajihusisha na vitendo hivyo wao kwa wao ili kutafuta umaarufu, wanachofanya ni kutojiamini na pia ni ushamba," amesema Riyama.

Kadhalika msanii huyo amewataka wasanii wasidhalilishane wao kwa wao na pia wajitahidi kutengeneza filamu zitakazowapaisha.

Msanii huyo amesisitiza kuwa nidhamu katika kazi za sanaa ndiyo itasaidia wasanii kufanikiwa na siyo vinginevyo.



# DUDU BAYA AJIRUDI

Na Mary Kadoke

HATIMAYE Dudu Baya Al-Maarufu kama Konki amemuomba radhi marehemu Rugemalila pamoja na ndugu, jamaa na marafiki juu ya madai yake kuwa alikuwa mnyonyaji.

Akizungumza na Alasiri Online amesema amefikia maamuzi hayo baada ya kutafakari kuwa si vyema kuendelea kuweka vinyongo hasa katika kipindi hiki cha 'Kwaresma'.

"Ni maamuzi tu niliyoamua kufanya, baada ya kuona kuwa si vyema kuendelea kubeba kinyongo katika kipindi hiki cha kwaresma," amesema.

Hivi karibuni kupitia ukurasa wake @ dudubayatz alituma kipande cha video kinachoonesha akijutia kauli zake za unyonyaji juu ya aliyekuwa mkurugenzi wa vipindi na uzalishaji wa Clouds marehemu Ruge.

Malalamiko aliyotoa Dudu kwa Ruge na watangazaji wa kipindi cha Extra, Extra Large (XXL) ni kukithiri kwa rushwa pale wasanii walipotaka kuachia ngoma zao.

Akimaanisha kuwa wasanii walitakiwa kutoa kidogo ili ngoma zao mpya ziende hewani.

Kifo cha Ruge kilisababishwa na tatizo la figo na kufariki Februari 26 mwaka huu akiwa Afrika Kusini alipokuwa anapatiwa matibabu.

# TUPA NA WOSIA KWA BONGO FLEVA

Na Anaeli Mbise

**MPULIZA midomo ya bata (saxophone) wa bendi ya Vijana Jazz Abdallah Tuba amerusha mawe kuwa wanamuziki wa siku hizi hawatungi nyimbo ambazo zinagusa hisia za watu kama walivyokuwa wanafanya katika muziki wa dansi.**

**Akizungumza na Alasiri Online, Tuba amesema kuwa mashairi mengi ya wanamuziki wa kileo yamekosa uhalisia wa mambo ambayo yanatokea katika jamii na kuishia kutunga nyimbo za kawaida.**

**Ukikuta zamani bendi inatunga wimbo wenye uhalisia kama vile Vijana nakumbuka tuliwahi kuwa na wimbo unaitwa Chiku ulizungumzia namna mtu anakufa angali kijana na katika jamii anapendwa kutokana na uchapaji kazi, lakini siku hizi mapenzi tu, amesema Tuba.**

**Kadhalika mwanamuziki huyo amesema kutokana na kubadilika kwa mazingira ya teknolojia kumechangia vijana wengi kutojiongeza ili kupata muziki bora.**

**Aidha msanii huyo amewataka wasanii wa kizazi kipya kufanya muziki kwa kutumia ala za muziki ili kujiimarisha vizuri zaidi.**

**Bendi ya Vijana jazz ilikuwa ikiongozwa na marehemu Hemed Maneti ikitesa na ngoma kama Bujumbura, Tanga, Ngoma, Jiko Limenuna, Lifti na Mwisho wa Mwezi.**



# LUIZA MBUTU
## ATAKA KUWA BI KIDUDE

Na Anaeli Mbise

**MUIMBAJI wa bendi ya Twanga Pepeta Luiza Mbutu, amefunguka kwamba kama Mungu ataendelea kumjalia kuwa hai atazeekea katika fani kama ilivyokuwa kwa Bi. Kidude.**


**Akizungumza na Alasiri Online, mwanamuziki huyo amesema kuwa kazi ya muziki mtu atafanya hadi pale Mungu ataamua kumchukua tu.**

**"Kwa sasa nina miaka 21 kwenye fani na sitaraji kustaafu kwa sababu kuimba hakuna umri, mbona Bi. Kidude alifariki akiwa bado anaimba? Na mimi nitafanya hivyo iwapo Mungu atanijalia kuwa hai,"amesema Mbutu.**

**Mwanamuziki huyo amesema haoni sababu ya kumfanya apumzike muziki haraka wakati kazi ya kuimba siyo ngumu kama unenguaji, ambako unafika wakati viungo vya msanii vinahitaji kupumzika.**

**Mwanamuziki huyo amedumu na bendi ya Twaga Pepeta kuanzia mwaka 2001 hadi sasa.**





# NEDY

## AAMUA KUBEBA CHIPUKIZI

Na Anaeli Mbise

MSANII wa muziki wa Bongo fleva Nedy Music ametangaza kuwa mwaka huu ameandaa tamasha la muziki la 'Welcome Home' ambalo atazunguka visiwani Zanzibar akiwa na wasanii tofauti tofauti.

Nedy akizungumza na Alasiri Online, amesema kuwa lengo la tamasha hilo ni kunyanyua wasanii wachanga kutoka visiwani Zanzibar.

"Nitazunguka nchi yote ambako nilizaliwa ili kukusanya vipaji vya kuimba na kusaidia mmoja baada ya mwingine ambaye atakuwa anafanya vizuri," amesema Nedy.

Aidha mwanamuziki huyo ameongeza kuwa kazi za sanaa ni za kusaidiana ili kuukuza muziki kibiashara na kimataifa.

Kwa upande mwingine, Nedy amempongeza Ommy Dimpoz kwa kurudi vizuri kwenye game baada ya kukaa kimya kwenye muziki kutokana na maradhi yaliyokuwa yanamsumbua.

# DDC MLIMANI KUSHAMBULIA PASAKA



Na Anaeli Mbise

BENDI kongwe ya muziki wa dansi nchini DDC Mlimani Park, itafanya tamasha la aina yake katika ukumbi wa Bajeti Resort ulioko Kunduchi jijini Dar es Salaam, siku ya Jumapili ya Pasaka.

Akizungumza na Alasiri Online, mratibu na mchambuzi wa muziki wa dansi Rajabu Zomboko amesema kuwa tamasha hilo litakuwa la kitofauti kutokana na kujumuisha wanamuziki wakongwe ambao waliwahi kuimba katika bendi hiyo.

Zomboko amesema miongoni mwa wanamuziki hao ni pamoja na Fresh Jumbe, Cosmas Chidumule pamoja na Benovila Anthony.

"Siku hiyo tutawaona manguli kama Cosmas Chidumule ambaye sasa ameokoka tumemuomba ila pia Fresh Jumbe na wengine wengi kina Max Bushoke wote hao," amesema Zomboko.

Kwa upande wake kiongozi wa bendi hiyo Abdallah Hemba ameongeza kuwa mashabiki wa Sikinde watarajie kupata zile ngoma ambazo zilitawala sana miaka ya 1978 mpaka 1982.

Miongoni mwa ngoma zilizotikisa ni pamoja na Gama, Nawashukuru Wazazi, Asha na Majirani Huzima Redio.